HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

MPANGO WA UANZISHAJI NA UENDELEZAJI VIWANDA ILI KUFIKIA UCHUMI WA KATI IFIKAPO MWAKA 2022

Utangulizi:

Serikali ilifanya uzinduzi rasmi wa Mkakati wa uanzishwaji wa viwanda 100 vidogo na vya kati kila Mkoa chini ya Kauli Mbiu **'MKOA WETU VIWANDA VYETU'** tarehe 09/11/2017 iliyoandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI)

Mgeni rasmi kwenye uzinduzi huo alikuwa Mhe. Selemani Jafo (MB) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI) pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Vijana na Watu wenye Ulemavu Mhe.Jenister Mhagama (MB), Naibu Waziri wa Viwanda Mhe.Mhandisi Stella Manyanya (MB), na Naibu Waziri OR TAMISEMI Mhe. Joseph G. Kakunda (MB) walikuwepo.

Wengine waliohudhuria ni Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI), Wakuu wa Mikoa wa Dodoma, Manyara, Singida, Morogoro na Wakurugenzi mbalimbali toka Wizara za Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI), Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma Wakuu wa Wilaya Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi za Mikoa na Wilaya Tanzania Bara.

LENGO LA MKAKATI

Kuhakikisha kila Mkoa kwa kutumia mbinu zake unaazisha na kuendeleza viwanda 100 vidogo na vya kati katika mwaka mmoja Desemba 1,2017 hadi Desemba 1,2018.

MAELEKEZO YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR TAMISEMI) JUU YA MKAKATI

- Mifuko 19 inayojihusisha na Hifadhi ya Jamii ijibu hoja ya nchi kuwa na viwanda

- Wakuu wa Mikoa wote wahamasishe uanzishaji wa viwanda vidogo na vya kati ya tarehe 01/12/2017 mpaka 01/12/2018
- Wakuu wa Mikoa wote wahakikishe maeneo ya ardhi kwa ajili ujenzi wa viwanda yanatolewa katika Mamalaka za Serikali za Mitaa
- Fedha za wanawake na vijana asilimia 10 zinazotengwa na Mamalaka za Serikali za Mitaa zitumike kwa kuanzisha viwanda kinachotakiwa ni kutoa uongozi (leadership) kwa maana ya maamuzi ya kifkra na mtazamo
- Maafisa Maendeleo ya Jamii kama mawakala wa mabadiliko wasimamie kampeni hii na kuwa na mpango kazi
- Bodi ya Mikopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGLB) ikopeshe Mamalaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuanzisha viwanda
- Katika kampeni hii Maafisa Maendeleo ya Jamii na viongozi wengine wafanye kazi ili waache alama (legacy) katika maeneo yao kuwa kazi ilifanywa na wao kuacha kufanya kazi kwa mazoea (business as usual)
- Mikoa 3, Wilaya 3 na Maafisa Maendeleo ya Jamii watatu (3) itakayofanya vizuri Serikali itatoa zawadi.

UZINDUZI WA MKAKATI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI) alizindua Mkakati kwa kukabidhi vitendea kazi kwa **Mkuu wa Mkoa**, Mkuu wa Mkoa alimkabidhi **Mkuu wa Wilaya**, **Mkuu wa Wilaya** alimkabidhi **Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri** na **Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri** alimkabidhi **Afisa Maendeleo ya Jamii** kuwakarishwa na Viongozi wa Mkoa wa **Dodoma** na Wilaya ya **Bahi**.

Hata hivyo Mwogozo rasmi wa utekelezaji wa Mkakati wa Uanzishwaji wa Viwanda 100 vidogo na vya kati kila Mkoa haukutolewa kilichokabidhiwa ilikuwa format ya Kuandaa mpango wa uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati kwa kushirikisha wadau na Sekta mbalimbali

MAJUKUMU YA HALMASHAURI YA WILAYA KATIKA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA UANZISHWAJI WA VIWANDA

i. Kuandaa na kuwa na Mpango Kazi wa kuhamasisha wananchi na wadau kushiriki uanzishaji na uendelelezaji viwanda vidogo na vya kati na kupata ridhaa ya Mamlaka husika.
ii. Kufanya tathmini ya hali ya viwanda katika Halmashauri ya Wilaya
iii. Kutekeleza ipasavyo Mpango Kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati utakaowezesha Wilaya kuwa na mchango kwenye uanzishaji viwanda 100 katika Mkoa

MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI YA MPANGO WA UTEKELEZAJI MKAKATI

Menejimenti imeandaa mapendekezo ya Mpango unaolenga kutekeleza Mkakati wa kuanzisha Viwanda vidogo na vya kati vipatavyo 30 ifikapo Desemba 2018 ambapo viwanda vinavyolengwa kwa mujibu wa Wizara ya Viwanda ni:

- Vile vyenye uwezo wa kuajiri watu hadi wane (4) na mtaji wake wa kuanzishwa ni chini ya TShs 5,000,000/=
- Aina nyingine ya viwanda ni vile vyenye uwezo wa kuajiri watu 5 hadi 50 na vinaweza kuwa na mtaji hadi TShs 200,000,000/=
- Viwanda vinaweza kuwa vya usindikaji vyakula, uchomeleaji vyuma, ukamuaji mafuta kutokana na mazao, utengenezaji magari, useremala, vyerehani vitano na zaidi, utengenezaji wa bidhaa za ngozi, ufyatuaji matofali kwa mashine, mashine za kusaga na kukoboa na ufungashaji asali

Naomba Kamati yako iyajadili mapendekezo ya kuanzisha viwanda vidogo na vya kati chini ya Kauli Mbiu ya **'MKOA WETU VIWANDA VYETU'** na kutoa ushauri wake ili uweze kuwasilishwa kwenye Baraza la Madiwani kwa uamuzi.

Naomba kuwasilisha,

Khamlo M.Njovu
Kny Mkurugenzi Mtendaji (W)
MPWAPWA

MAPENDEKEZO YA MPANGO KAZI WA UANZISHAJI NA UENDELEZAJI VIWANDA ILI KUFIKIA UCHUMI WA KATI IFIKAPO MWAKA 2022

LENGO KUU:

Wilaya ya Mpwapwa Kuwa na uchumi wa Kati na wa Viwanda ifikapo Desemba 2022.

LENGO MAHUSUSI:

1. Kuwa na Viwanda vipya 13 ifikapo Desemba 2018.
2. Kuongeza uzalishaji Malighafi zitakazotumika katika viwanda ifikapo Desemba 2018.
3. Ufuatiliaji na tathmini ya uanzishwaji wa viwanda ifikapo Desemba 2018.

Eneo la utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2018

Na	TARAFA	Na	KATA	Na	VIJIJI
1	Mpwapwa Mjini	1	Mpwapwa Mjini	1	
				2	
		2	Kimagai	3	
				4	
2	Kibakwe	3	Kibakwe	5	
				6	
		4	Pwaga	7	
				8	
3	Mima	5	Mima	9	
				10	
		6	Berege	11	
				12	
4	Rudi	7	Rudi	13	
				14	
		8	Mtera	15	
				16	

Viatarishi vinayoweza kufanya Mpango usitekelezeke

1. Ukinzani wa kisiasa katika kuanza kutekeleza mradi au maeneo ya kipaumbele.

2. Kutokuwa na ushirikiano kwa wadau na ukosefu wa uratibu wa shughuli.
3. Ukosefu wa fedha za Utekelezaji wa Mpango
4. Utekelezaji hafifu wa Mpango

Mambo yanayoweza kusaidia kufanikisha kwa Mpango

1. Mapokeo chanya na kupitishwa na viongozi wa kisiasa, kukubalika na Serikali, uwajibikaji wakati wa utekelezaji wa Mpango.
2. Ushiriki wa wadau mbalimbali katika kufadhili na kutekeleza Mpango
3. Upashanaji wa habari za utekelezaji, ufuatiliaji wa changamoto na utatuzi katika ngazi zote za utekelezaji.
4. Ufuatiliaji wa karibu na wa mara kwa mara wa utekeleaji wa Mpango kwa muda muafaka.
5. Kuepuka viatarishi ambavyo vitasababisha Mpango usitekelezeke
6. Ufuatiliaji, tathmini, utoaji wa taarifa za utekelezaji na Usimamizi wa Mpango.

Wadau wa Utekelezaji wa Mpango

1. TAMISEMI
2. Idara kuu ya Maendeleo ya Jamii Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
3. Sektretarieti ya Mkoa
4. Halmashauri ya Wilaya
5. Asasi za kiraia
6. Sekta binafsi
7. Wadau wa Maendeleo
8. Taasisi za Elimu
9. Vikundi vya uzalishajimali vya kijamii
10. Jamii